TANGAZO LA SERIKALI NA. 123 la tarehe 23/2/2024

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

## AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MRADI WA USIMAMIZI WA MRADI WA UJAZILIZI WA UMEME VIJIJINI MZUNGUKO WA IIB WA KAMPUNI YA MULTICONSULT NORGE AS YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Mradi wa Usimamizi wa Mradi wa Ujazilizi wa Umeme Vijijini Mzunguko wa IIB wa Kampuni ya Multiconsult Norge As ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 19 Disemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa gari lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii, lililoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na kampuni ya Multiconsult Norge As kwa ajili ya mradi wa usimamizi wa mradi wa ujazilizi wa umeme vijijini mzunguko wa IIB unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba msamaha katika Amri hii haujatolewa ikiwa gari litatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yaliyotolewa na

Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 16 Juni, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| No. | MAELEZO | NAMBA YA CHESESI | NAMBA YA INJINI |
|---|---|---|---|
| 1 | NISSAN TERRS STATION WAGON | MNTJCD23Z0006167 | YD25030137U |

Dodoma,
14 Februari, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*